Haliuzwi


OKTOBA 15, 2025

# IMAAN

ISSN 5618 - NO. 554

Huwatoa watu gizani kwa idhini ya Allah

## Aref Nahdi arejea uwekahazina BASUTA na mikakati 3 kiuchumi



# Mafanikio lukuki BASUTA ikitimiza miaka 17

- Yatoa tamko kuukemea wanaohatarisha amani
- Yasuka safu mpya ya viongozi
- Masheikh wataja matamanio yao kwa BASUTA mpya HABARI UK. 2 - 7



Mapitio ya Kitabu
Nasaha za wiki
Visa vya Mitume na Maswahaba
Matukio Yenye Mazingatio

## Tafakuri juu ya benki ndogo za Kiislamu kuhusu maadili na ujumuishaji wa kifedha

## Mwinyi apongeza kuanzishwa kwa Jumuiya ya Walimu wa Madrasa

- Asisitiza viongozi wa dini, wanasiasa na waandishi wa habari kuhubiri amani wakati wote HABARI UKURASA 3



## Vita yasitishwa Gaza kuruhusu mwanga wa matumaini




HABARI MOROGORO

NA YUSUPH AMIN

# Mafanikio lukuki BASUTA ikitimiza miaka 17

Naibu Katibu Mkuu wa Baraza Kuu la Jumuiya za Ansaar Sunnah Tanzania (BASUTA), Sheikh Mohamed Issa, amesema katika kipindi cha miaka 17 ya Baraza hilo hatua kubwa na thabiti ya mafanikio imepigwa katika maeneo kadhaa ikiwamo kuimarisha uhusiano wa kimataifa kupitia ushirikiano na mabalozi wa nchi mbalimbali na taasisi za Kiislamu duniani kote.

Sheikh Issa ameyasema hayo Jumamosi iliyopita wakati wa Mkutano Mkuu wa BASUTA uliofanyika kwenye Ukumbi wa Mikutano wa Kimataifa wa Mwalimu Nyerere (JNICC) jijini Dar es Salaam.

Akisoma taarifa ya utendaji wa BASUTA katika kipindi cha kuanzia mwezi Januari 2008 hadi Septemba 2025, Sheikh Issa alisema kupitia ushirikiano huo baadhi ya wanajumuiya waliweza kutekeleza ibada za Umra na Hijja kwa ufadhili wa Serikali ya Saudi Arabia, pamoja na kushiriki mikutano ya kimataifa ya kidini na mafunzo ya kiutawala, kujenga uhusiano wa kidiplomasia na kuendeleza elimu na maadili ya Kiislamu kwa jamii ya Watanzania.

"BASUTA ilipokea mwaliko tarehe 23 Septemba 2017 kupitia Ofisi ya Katibu Mkuu kushiriki ibada ya Hijja, safari ambayo ilifadhiliwa kikamilifu na Muslim World League, ikiwa ni sehemu ya juhudi za kuimarisha mshikamano wa Kiislamu duniani," alieleza Sheikh Issa.

Alitaja mafanikio mengine kuwa ni taasisi kuu za BASUTA kama vile The Islamic Foundation (TIF) na Ansaar Muslim Youth Center (AMYC) kuchangisha fedha kwa ajili ya kusaidia waathirika wa majanga mbalimbali na matibabu.

Katika misaada hiyo, The Islamic Foundation pekee walitoa kiasi cha shilingi bilioni 2 na milioni 310 za Kitanzania kwa ajili ya kuwasaidia waathirika wa majanga mbalimbali hapa nchini na nje ya nchi, hususan wananchi wa Gaza.

Pia, katika kipindi hicho miongoni mwa taasisi za BASUTA zilitoa huduma za matibabu (kambi za matibabu) bure kwa kushirikiana na hospitali za Serikali kama vile Taasisi ya Moyo ya Jakaya Kikwete (JKCI) na Hospitali za Rufaa za Mikoa kwa wagonjwa wa moyo, macho na mengineyo.

Kwa upande wa elimu ya dini, hadi sasa taasisi zilizo chini ya BASUTA zinamiliki Maahad za elimu ya dini, ambapo kwa upande wa Ibtidaaiya zipo 68, Mutawasitwa 31, Thanawi nane, madrasa za misikitini 1476 na Tahfidhul Qur'an sita. Kwa upande wa huduma za jamii, kufikia sasa baadhi ya taasisi za BASUTA zimeshachimba jumla ya visima vifupi na virefu 3,608 na zina yatima 52 wanaolelewa nyumbani na 1964 kwenye vituo mbalimbali.

Mafanikio mengine yaliyopatikana ni kushiriki kutoa maoni katika uandaaji wa Dira ya Taifa 2050.

Sheikh Issa alisema, katika kutambua mchango wa BASUTA, mwaka huu wa 2025, Waziri wa Mipango na Uwekezaji, Prof. Kitila Mkumbo, katika hotuba yake ya bajeti aliitaja BASUTA kama mdau muhimu katika kutoa maoni juu ya Dira ya Taifa 2050.

Aidha, katika kipindi cha miaka 10 kuanzia 2016 hadi 2025, Baraza limepiga hatua kubwa katika kuimarisha uhusiano wa kimataifa, jambo ambalo limekuwa na matokeo chanya kwa taasisi na wanajumuiya kwa ujumla.

Sheikh Muhammad amesema BASUTA inaendelea kujizatiti kuendeleza ushirikiano na taasisi za ndani na nje ya nchi kwa maslahi mapana ya Uislamu na jamii ya Watanzania.

**■ Mafanikio mengine kuwa ni taasisi kuu za BASUTA kama vile The Islamic Foundation (TIF) na Ansaar Muslim Youth Center (AMYC) kuchangisha fedha kwa ajili ya kusaidia waathirika wa majanga mbalimbali na matibabu. Katika misaada hiyo, The Islamic Foundation pekee walitoa kiasi cha shilingi bilioni 2 na milioni 310 za Kitanzania kwa ajili ya kuwasaidia waathirika wa majanga mbalimbali hapa nchini na nje ya nchi, hususan wananchi wa Gaza.**

## Sekta ya elimu

Katika nyanja ya elimu, BASUTA imekuwa mshirika mkubwa wa Wizara ya Elimu katika masuala mbalimbali ya elimu ya mazingira.

Mussa Buluki, Mkurugenzi wa Idara ya Elimu – BASUTA amesema kuwa, BASUTA kama mjumbe wa mikutano mbalimbali ya Kamati ya Maendeleo ya Sekta ya Elimu (ESDC) imekuwa ikifuatilia utekelezaji wa mipango yote ya sekta ya elimu na kupitisha na kuidhinisha sera zote za sekta, mikakati, mipango, programu, miongozo na ripoti.

Kwa mujibu wa Buluki, katika mwaka 2024 na 2025 pekee, BASUTA imeshiriki vikao vyote vya kamati.

Mikutano mingine ambayo BASUTA imewahi kushiriki ni ule wa Mapitio ya Pamoja ya Sekta ya Elimu ya Mwaka kujadili mafanikio na changamoto zilizobainishwa na wadau mbalimbali katika utekelezaji wa programu na mikakati ya elimu.

Tangu kuundwa kwake mwaka 1995, BASUTA imekuwa mojawapo ya taasisi shiriki za Umoja wa Wamiliki wa Shule zisizo za Kiserikali nchini (TAMONGSCO).

Vilevile, BASUTA ipo katika kamati ya kuendeleza sekta ya elimu nchini na imekuwa ikishiriki kwenye vikao vya Halmashauri Kuu ya TAMONGSCO tangu mwaka 2016 hadi sasa, hivyo kutoa mchango wake katika kuendeleza sekta ya elimu nchini.

## Ushirikiano mpya 2025

Katika mwaka 2025, BASUTA ilifungua ukurasa mpya wa ushirikiano na Sheikh Bilali Ismail kutoka Shirika la Imam Development Program la nchini Afrika Kusini.

Sheikh Bilali alifika nchini na kuzuru ofisi za BASUTA katika ziara iliyolenga kujenga uhusiano mpya na kubadilishana uzoefu kuhusu utekelezaji wa miradi ya maendeleo ya viongozi wa dini barani Afrika.

Mkutano Mkuu wa mwaka wa BASUTA ulihudhuriwa na wajumbe pamoja na wawakilishi kutoka taasisi mbalimbali zilizo chini ya BASUTA, ikiwamo The Islamic Foundation (TIF), Ansaar Muslim Youth Center (AMYC), Alwahda Mission Islamic, Al-Azizu Islamic Center, na Daarul Uluum Islamiyyah.

Taasisi nyingine ni Arusha Ansaru Sunnah Association, Darul Hijrah Islamic Center, Islamic Center of Mbinga, na Darul Hadith Salafiyah.




**HABARI ZANZIBAR**

NA YUSUPH AMIN

## KUELEKEA UCHAGUZI MKUU:

# BASUTA yatoa tamko kuukemea wanaohatarisha amani nchini



Baraza Kuu la Jumuiya za Ansaar Sunnah Tanzania (BASUTA) limekemea watu wanaotumia vibaya uhuru wa kujieleza, tabia ambayo inahatarisha amani na utulivu wa nchi.

Kauli hiyo imetolewa na Katibu Mkuu wa Baraza hilo, Sheikh Shaaban Mussa katika Mkutano Mkuu wa taasisi hiyo uliofanyika kwenye Ukumbi wa Mikutano wa Kimataifa wa Mwalimu Nyerere (JNICC), jijini Dar es Salaam.

Akisoma tamko la BASUTA kwa niaba ya uongozi wa taasisi hiyo, Sheikh Shaaban amewahimiza wananchi wote kushiriki kikamilifu katika zoezi la kupiga kura mnamo tarehe 29, Oktoba na kurejea nyumbani kwa amani na utulivu kusubiri matokeo.

Katika tamko hilo lenye kurasa mbili, Sheikh Shaaban alionya tabia ya baadhi ya watu wanaotumia mitandao ya kijamii kusambaza propaganda za kichochezi, kuhamasisha maandamano haramu, kuzua taharuki, au kuhatarisha mshikamano wa kitaifa.

Alisema kufanya vurugu si njia ya haki, bali ni mtego wa kuangamiza amani. "BASUTA inawakumbusha wananchi kwamba iwapo kutatokea kutoridhika kwa mtu yeyote kuhusu hatua yoyote ya mchakato wa uchaguzi; iwe inahusu kazi ya Tume, vyama vya siasa au matokeo yatakapotangazwa, basi mlango wa sheria uko wazi. Mtu huyo ana haki ya kikatiba ya kuwasilisha malalamiko yake kwenye vyombo husika vya sheria, si kujiingiza katika vitendo vya uchochezi au uvunjifu wa amani.

"BASUTA inasisitiza kwamba amani yetu haipaswi kufananishwa na kichwa cha mwehu – kisichojali wala kuelewa. Amani ni hazina adhimu inayopaswa kulindwa kwa nguvu zote," alisema.

Sheikh Shaaban alibainisha kuwa, himizo la mafundisho ya Uislamu la kuamrisha mema na kukataza maovu, si kwa sababu ya kujipendekeza kwa wenye mamlaka bali ni wajibu wa kijamii unaolenga kuokoa watu wote (watawala na watawaliwa).

Alisema ni wajibu kushughulikia maovu mapema kabla hayajaangamiza watu wote, huku akinukuu maneno ya mwanachuoni Al–Muhallab yanayosema, "Iwapo jamii itaunyamazia uovu wa wachache, basi adhabu yake itawaumiza wote."

> **"BASUTA inasisitiza kwamba amani yetu haipaswi kufananishwa na kichwa cha mwehu – kisichojali wala kuelewa. Amani ni hazina adhimu inayopaswa kulindwa kwa nguvu zote**
>
> KATIBU MKUU BASUTA, SHEIKH SHAABAN MUSSA

Aidha, BASUTA imetoa wito kwa viongozi wa dini, wanasiasa, vijana, na wananchi kwa ujumla kujiepusha na kauli za uchochezi na kuhamasisha vurugu.

بِسۡمِ ٱللَّهِ ٱلرَّحۡمَـٰنِ ٱلرَّحِيمِ

# TAMKO LA BASUTA KUELEKEA UCHAGUZI KUHUSU KUHIFADHI AMANI LILILOTOLEWA KWENYE MKUTANO WAKE MKUU MBELE YA WAANDISHI WA HABARI

Baraza Kuu la Jumuiya za Ansaar Sunna Tanzania (BASUTA), likiwa ni taasisi ya dini inayojikita katika kuhimiza amani, maadili mema, na mshikamano wa kitaifa, leo mwezi 19 Rabiul Akhir mwaka 1447 Hijiria, sawa na tarehe 11/10/2025, linatoa tamko hili maalumu kuelekea uchaguzi Mkuu unaotarajiwa kufanyika hivi karibuni.

Tarehe 29 Oktoba mwaka huu 2025, ni siku ya uchaguzi wa madiwani na wabunge kwa Tanzania bara lakini madiwani, wawakilishi na Rais wa Zanzibar kwa Tanzania visiwani. Kwa Tanzania nzima, pia Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania naye atapigiwa kura.

Kwa kawaida zoezi la uchaguzi ni tukio nyeti kwenye nchi yoyote - kama halikufanyika kwa umakini na kutanguliza mbele maslahi ya taifa, mara nyingi hupelekea katika uvunjifu wa amani na hata kulitumbukiza taifa katika janga la machafuko na wakati mwingine vita - Mwenyezi Mungu atulinde na majanga hayo.

BASUTA inawahimiza wananchi wote kushiriki kikamilifu katika zoezi la kupiga kura kwa amani, kurejea nyumbani kwa utulivu, na kusubiri matokeo kwa subira bila ya jazba wala mihemko isiyo ya lazima. Ni muhimu tukatambua kuwa kuna maisha kabla, wakati na baada ya uchaguzi. Kwa msingi huo, kuilinda amani ni jukumu la kila raia kwa ajili ya mustakabali wa taifa letu na vizazi vijavyo.

BASUTA inawakumbusha wananchi kwamba iwapo kutatokea mtu yoyote kutoridhika kuhusu hatua yoyote ya mchakato wa uchaguzi, iwe ni kuhusu kazi ya Tume, vyama vya siasa au matokeo yatakapotangazwa; basi mlango wa sheria uko wazi. Mtu huyo ana haki ya kikatiba ya kuwasilisha malalamiko yake kwenye vyombo husika vya sheria, na si kujiingiza katika vitendo vya uchochezi au uvunjifu wa amani.

Aidha, BASUTA inapinga vikali tabia inayoanza kushika kasi ya matumizi mabaya ya uhuru wa mawazo na kujieleza, hasa kupitia mitandao ya kijamii, ambapo baadhi ya watu wanatumia majukwaa hayo kusambaza propaganda za kichochezi, kuhamasisha maandamano haramu, kuzua taharuki, na kuhatarisha mshikamano wa kitaifa. Hizi si njia za haki, bali huu ni mtego wa kuangamiza amani yetu sote.

Tukumbuke kauli ya Mtume Muhammad ﷺ alivyosema, kama ilivyoripotiwa na Imamu Muslim kutoka kwa Swahaba Jabir Allah (amridhie):

"Hakika shetani amekata tamaa ya kuabudiwa na wanaoswali kwenye Ghuba ya Waarabu, lakini ameweka juhudi zake katika kuwachonganisha wao kwa wao."

Ujumbe huu ni onyo na mazingatio kwa jamii kwamba shetani hatatumia tena njia ile ya ibada kuwapoteza watu wa dini, bali atatumia njia ya propaganda, uongo, mabishano, uchochezi, matusi, chuki, migawanyiko na fitna, hasa katika nyakati nyeti kama hizi.

BASUTA inasisitiza kwamba amani yetu haipaswi kufananishwa na kichwa cha mwehu – kisichojali wala kuelewa. Amani ni hazina adhimu inayopaswa kulindwa kwa nguvu zote. Uislamu umetufundisha na kututahadharisha kuwa sumu haionjwi. Na suala la kuamrisha mema na kukataza maovu ni wajibu wa kijamii unaolenga kutuokoa sote: watawala na watawaliwa.

Mtume Muhammad ﷺ, alitoa mfano mzito katika hadithi ya jahazi: "Mfano wa watu waliomo kwenye jahazi – baadhi yao wako juu na wengine chini. Wale wa chini walipohitaji maji, walipaswa kupita juu, na hilo likawa kero kwa walioko juu. Wakawaza kutoboa chini ya jahazi ili wapate maji moja kwa moja. Wakiachiwa, wote watazama; wakizuiwa, wote watanusurika." (Bukhariy)

Hadithi hii inaelekeza wajibu wa kushughulikia maovu mapema kabla hayajaangamiza wote. Na kama walivyoeleza baadhi ya wanazuoni kama Al-Muhallab رحمه الله: "Iwapo jamii itaunyamazia uovu wa wachache, basi adhabu yake itawaumiza wote."

Kwa msingi huu:

BASUTA inatoa wito kwa viongozi wa dini, wanasiasa, vijana, na wananchi kwa ujumla kuhakikisha wanakuwa walinzi wa amani, si wachochezi wa migogoro.

Tusikubali makundi ya watu wachache kulivuruga jahazi letu la taifa.

Tuchague amani, tukatae chuki.

Tukemee fitna na tusimamie haki kwa njia halali.

Mwisho, tukumbuke:

11/10/2025

"Ikiwa tutanyamaza mbele ya uovu, basi madhara yake hayataishia kwa wakosaji tu, bali jamii nzima itaumia."

Wabillahi taufiq.

*Wasalaamu alaykum wa rahmatullahi wa barakaatuh*

NA YUSUPH AMIN

# DC Kinondoni: Wananchi mkachague viongozi bora kwa amani

Suala la amani na utulivu kuelekea Uchaguzi Mkuu 2025 ni miongoni mwa yaliyozungumzwa katika Mkutano Mkuu wa Baraza Kuu la Jumuiya za Ansaar Sunnah Tanzania (BASUTA), uliofanyika Oktoba 11, 2025 kwenye Ukumbi wa Mikutano wa Kimataifa wa Mwalimu Nyerere (JNICC), jijini Dar es Salaam.



Mgeni rasmi kwenye Mkutano huo, Mkuu wa Wilaya ya Kinondoni, Saad Mtambule, aliyemuwakilisha Mkuu wa Mkoa, Albert Chalamila, amewasisitiza Waislamu na jamii kwa ujumla kudumisha amani na mshikamano kwani amani ndiyo msingi wa maendeleo ya mtu mmoja mmoja, jamii na Taifa.

Vilevile amewasihi wananchi kuchagua viongozi bora watakaofanya amani na utulivu viendelee kuwepo nchini.

Mtambule alitolea mfano migogoro inayoendelea nchini Jamhuri ya Kidemokrasia ya Congo (DRC), Msumbiji na Burundi kuwa ni matokeo ya kukosekana kwa amani.

"Kuna wimbi la wahamiaji kutoka nchi mbalimbali ikiwamo Msumbiji na Burundi. Katika kata ya Tandale pekee kuna wahamiaji 80, na kata ya Kawe ina wahamiaji 75, hivyo kuweni macho na kuwapokea wageni msiowajua... na hata ukiwauliza kwanini mnapenda kuja Tanzania wanakuambia Tanzania ni nchi ya amani," alisema Mtambule na kuongeza:

"Nafasi yoyote uliyokuwa nayo hakikisha unaitumia vizuri katika kulinda amani, kuchochea maendeleo na uchumi ili kumcha Mwenyezi Mungu kisawasawa."

## Aipongeza BASUTA

Aidha, Mkuu huyo wa wilaya ameipongeza BASUTA na kusema kuwa Serikali inatambua na kuthamini kazi kubwa wanayoifanya.

Katika nyanja ya elimu, Mtambule amesema ni muhimu kwa taasisi kuendelea kuwasisitiza Waislamu juu ya kushika elimu zote mbili – ya dini na mazingira.

Ameongeza kuwa ili Uislamu uendelee kushamiri ni lazima kuisoma Qur'an na kuielewe, lakini pia kusoma elimu ya mazingira. "Tusiposhika elimu dunia (ya mazingira) katika ulimwengu huu wa sayansi na teknolojia nguvu yetu itapungua," alionya Mtambule.

Kwa upande wake, Afisa Mfawidhi Msajili wa Jumuiya za kiraia Kanda ya Mashariki, Luko Mbwilo, ameukumbusha uongozi wa BASUTA kufanya kazi kwa kufuata sheria, kanuni na miongozo waliyojiwekea, na pia kuzingatia mifumo ya sheria za nchi.

"Msemaji aliyepita amezungumzia malengo ya BASUTA, ambayo ndiyo yalifanya BASUTA isajiliwe. Kwa hiyo hatutegemi kuwa tutatoka nje ya malengo yetu," alisema Luko.

Vilevile, ameelekeza kuwa vikao vya Baraza lazima viitishwe kwa mujibu wa Katiba, kadhalika viongozi wazingatie masharti ya usajili ikiwa ni pamoja na kulipa ada ya kila mwaka kwa wakati na kuwasilisha taarifa za mapato na matumizi, pamoja na taarifa za utendaji kwa msajili.

Luko alisema viongozi wengi wa taasisi, zikiwamo za Kiislamu wamekuwa wakikwepa kuitisha vikao na hivyo kusababisha migogoro na kutoelewana.



NA YUSUPH AMIN

# BASUTA wapata safu mpya ya viongozi




Baraza Kuu la Jumuiya za Ansaar Sunnah Tanzania (BASUTA) limekamilisha Mkutano wake Mkuu wa Mwaka jijini Dar es Salaam kwa kufanya uchaguzi wa viongozi katika ngazi mbalimbali.

Katika uchaguzi huo uliofanyika Oktoba 11, 2025, Sheikh Ally Zubeir alichaguliwa kuwa Amir wa Baraza hilo huku Sheikh Juma Ikusi akichaguliwa kuwa Naibu Amir.

Wengine waliochaguliwa ni Sheikh Shaaban Mussa (Katibu Mkuu), Sheikh Muhammad Issa (Naibu Katibu Mkuu) na Aref Nahdi (Mweka hazina), ambaye alipitishwa na wajumbe wote kwa kura za ndiyo.

Kwa upande wa wajumbe wa Baraza la Ulamaa la BASUTA, waliochaguliwa ni Sheikh Ally Zubeir, Sheikh Jabir Katura, Sheikh Salim Barahiyan, Sheikh Nassir Abdallah, Sheikh Twaha Bane, Sheikh Juma Poli, Sheikh Shaafi Mgaza, , Sheikh Waziri Maduga, Sheikh Shaaban Mussa, Sheikh Said Omar, Sheikh Yahya Hassan, Sheikh Ibrahim Abdulrahman, Sheikh Yahya Mrisho, Sheikh Khamis Mbonde, Sheikh Ally Nassor na Sheikh Zuberi Chunguru. Akifunga Mkutano huo, Amir mpya wa BASUTA, Sheikh Ally Zuberi aliwataka wajumbe wote kushirikiana na kushikamana katika kulijenga Baraza, na kudokeza kuwa BASUTA haina lengo la kupora mali za wanachama wake wala kushindana.



ربيع ثان

# HABARI
## DAR ES SALAAM

NA MWANDISHI WETU



■ Nahdi ambaye pia ni Mwenyekiti w The Islamic Foundation, alitangaza kufuta deni la shilingi Milioni 137 kwa Baraza Kuu la Jumuiya za Ansaar Sunna Tanzania (BASUTA) ilizozikopesha katika miaka mitano iliyopita.

# Aref Nahdi arejea uwekahazina BASUTA na mikakati 3 kiuchumi

Mweka Hazina wa Baraza Kuu la Jumuiya za Ansaar Sunna Tanzania (BASUTA), Aref Nahdi amerejeshwa tena katika nafasi hiyo huku akitangaza mikakati mitatu ya kuinua uchumi wa Baraza hilo.

Akizungumza wakati anawasilisha ripoti ya fedha ya miaka mitano iliyopita katika mkutano mkuu wa Baraza hilo uliofanyika Kituo cha Mikutano cha Kimataifa cha Julius Nyerere mwishoni mwa wiki, Nahdi alisema mikakati hiyo ni muhimu ili kuiwezesha taasisi hiyo kupata mapato yake na kujitegemea.

Alitaja mikakati hiyo kuwa ni pamoja na kuimarisha mifumo ya ukusanyaji mapato, kutafuta vyanzo mbadala na kutafuta jengo litakaloingizia mapato Baraza hilo.

Nahdi alisema: "Tukiangalia mbele kwa matumaini na msukumo mpya, tunapendekeza ... kuimarisha mfumo ya kujitolea na ukusanyaji wa ada au michango ya wanajumuiya kwa njia rahisi na uhakika; pili, kutafuta vyanzo mbadala vya mapato ikiwa ni pamoja na kushirikiana kuitafutia basuta watu wa kheri wa ndani na nje ya nchi wenye utayari wa kupitisha sadaka zao au sehemu ya fungu la zaka walilete kwa ajili ya kusaidia basuta na tatu, kunzisha mchakato wa kumiliki jengo la waqf la baraza liwezalo kuingiza mapato ya kudumu na kulifanya baraza liwe hai na lijitegemee."

Hata hivyo, Nahdi, alionya kuwa ili hayo yawezekane, wanachama lazima wawe tayari kujitolea wakielewa thamani ya baraza hilo kwa ustawi na maendeleo ya Wanasunna na taasisi za Kisunna Tanzania.

"Haya yote yatawezekana kama kila mmoja wetu atakuwa tayari kuliunga mkono (Baraza) kwa dhati, moyo, ari, muda, na kwa mali. Kumbukeni baraza hili ni dira ya umoja wetu, ni jukwaa la kushirikiana, kushauriana, na kusimamia masuala ya kimsingi ya jumuiya zetu zote za kisunna hapa nchini.

Nahdi aliwahamasisha wajumbe wa mkutano: Tunawasihi kwa moyo mkunjufu tuamke, tusimame, tuchangie na kila taasisi ihakikishe inakuwa sehemu ya kuchangia basuta. Tuache nena dhana kuwa kazi hii ni ya viongozi tu au taasisi fulani tu au watu wachache walioteuliwa au kuchaguliwa.

Awali katika utangulizi wa hotuba yake, Nahdi alisema zinapoanzishwa taasisi mfano wa Basuta, ni muhimu kufikiria namna ya kupata mapato ya kuwezesha shughuli zake badala ya kuishia kuweka mipango ya kazi tu.

Alisema rasilimali fedha ni muhimu ili kupata fedha za kulipia mambo ya msingi katika uendeshaji wa ofisi ikiwemo pango, posho za watendaji, gharama za mkutano ya kikatiba na vilevile kwa ajili ya kugharamia majukumu ya kazi yanayohuisha uhai wa taasisi kama semina, makongamano, warsha, na ziara matawini.

"Ndugu wajumbe, katika baraza letu kama kuna rasilimali watu lakini hakuna rasilimali fedha ujue hapo hakuna uhai," Nahdi alionya.

> "Ili hayo yawezekane, wanachama lazima wawe tayari kujitolea wakielewa thamani ya baraza hilo kwa ustawi na maendeleo ya Wanasunna na taasisi za Kisunna Tanzania.
>
> AREF NAHDI

Akirejea Qur'an Tukufu, katika Surat Tawba aya ya 41: "Na ipiganieni dini ya Allah kwa mali zenu na nafsi zenu. Hii ni kheri kwenu ikiwa mnajua," Nahdi alisema aya hiyo haitenganishi kati ya rasilimali watu na fedha – kama nguzo za kweli za kuipambania dini na kuendeleza taasisi zake.

"Kutoziunganisha nguvu mbili hizo ni kasoro kubwa," alisema Nahdi na akasisitiza tena: "Dhamira au kuwa na nia njema pekee hubaki kuwa ndoto (bila rasilimali fedha)."

Katika hotuba yake, Nahdi ambaye pia ni Mwenyekiti w The Islamic Foundation, alitangaza kufuta deni la shilingi Milioni 137 kwa Baraza Kuu la Jumuiya za Ansaar Sunna Tanzania (BASUTA) ilizozikopesha katika miaka mitano iliyopita.

ربيع ثان

**HABARI**
**DAR ES SALAAM**

NA MWANDISHI WETU



# Dkt. Mwinyi apongeza kuanzishwa kwa Jumuiya ya Walimu wa Madrasa

Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi, Mheshimiwa Dkt. Hussein Ali Mwinyi, amepongeza kuanzishwa kwa Jumuiya ya Walimu wa Madrasa na kuwataka kudumisha umoja.

Rais Dkt. Mwinyi ameyasema hayo, alipozungumza katika Dua Maalumu ya kumuombea yeye pamoja na kuliombea Taifa na Uchaguzi Mkuu ujao iliyofanyika Ukumbi wa Dkt. Ali Mohamed Shein, Tunguu, Mkoa wa Kusini Unguja.

Dkt. Mwinyi alijumuika na Walimu wa Madrasa, Masheikh na Uongozi wa Afisi ya Mufti Mkuu katika Dua Maalumu ya kuniombea pamoja na kuliombea Taifa na Uchaguzi Mkuu.

Dua hiyo imeandaliwa na Afisi ya Mufti kwa kushirikiana na Jumuiya ya Kuendeleza Walimu wa Vyuo vya Qur'an Zanzibar (JUKUWAVOQUZA)

Katika salamu zake amewakumbusha wananchi umuhimu wa kuiombea amani nchi ikielekea Uchaguzi Mkuu wa tarehe 29 Oktoba 2025.

Amesisitiza viongozi wa dini, wanasiasa na waandishi wa habari kuhubiri amani wakati wote.

Aidha Dkt. Mwinyi, amesema kuwa amani ni msingi wa maendeleo, na hakuna jambo muhimu zaidi kwa Taifa kuliko kuilinda na kuidumisha daima.






# Tafakuri juu ya benki ndogo za Kiislamu kuhusu maadili na ujumuishaji wa kifedha

Katika dunia yenye misukosuko ya kiuchumi na pengo kubwa kati ya matajiri na maskini, semina ya Profesa Dkt Rusni Hassan kuhusu "Kujenga ustahimilivu wa uchumi kupitia benki ndogo za Kiislamu" ilitoa mtazamo mpya na wenye kuhamasisha kuhusu namna fedha zinavyoweza kuhudumia binadamu.

Hotuba hiyo iliyotolewa katika Hoteli Indonesia Kempinski, Jakarta, tarehe 2 Oktoba 2025, ilionyesha jinsi kanuni za Kiislamu—adl (haki), amanah (uangalizi wa rasilimali), maslahah (maslahi ya umma), na rahmah (huruma)—zinavyoweza kuongoza uundaji wa mfumo wa kifedha jumuishi na wa kimaadili.

Kama mwanafunzi wa chuo, kusikiliza semina hii kulinipanua uelewa kwamba mifumo ya fedha inayozingatia imani inaweza kuleta suluhisho la kweli kwa changamoto za kiuchumi, hasa Kusini Mashariki mwa Asia ambako kuna ukosefu wa usawa na uhamaji mdogo wa kifedha.

Profesa Rusni alianza kwa kuchora taswira ya uchumi wa sasa. Akirejea utafiti wa Ipsos What Worries the World (2025), alieleza kuwa 63% ya watu duniani wanaamini nchi zao zinaelekea njia isiyo sahihi, wakihofia mfumuko wa bei, ukosefu wa ajira, na rushwa. Takwimu kuhusu ukosefu wa usawa wa utajiri zilishangaza: 1.6% ya watu duniani wanamiliki karibu nusu ya utajiri wote, huku mabilioni wakiwa na chini ya asilimia moja.

Hii ilionyesha kuwa mifumo ya sasa ya uchumi, licha ya maendeleo, bado imeshindwa kuleta haki na uwiano. Suala la ukosefu wa usawa si la kifedha tu bali pia la maadili. Uwasilishaji wa Profesa Rusni uliniunganisha na maadili ya msingi ya uchumi wa Kiislamu—kulinda hadhi, haki na huruma.

Kisha akaeleza jinsi fedha za Kiislamu zinavyotoa mbadala wa kina kwa mifumo ya kawaida. Badala ya kuangalia fedha kama chombo cha faida pekee, fedha za Kiislamu zinaunganisha shughuli za kiuchumi na uwajibikaji wa maadili. Malengo yake yanatokana na Maqasid al-Shariah: kulinda uhai, mali, akili, imani na heshima. Ukweli kwamba mali ya sekta ya fedha za Kiislamu ilifikia dola za Marekani trilioni 4.9 mwaka 2023 unaonyesha mwamko mkubwa wa fedha za kimaadili duniani.

Kabla ya semina, niliangalia fedha kama namba, uwekezaji na ukuaji tu. Baada ya kusikia maoni ya Profesa Rusni, niliiona fedha kama njia ya kutumikia haki ya kijamii. Alivyounganisha utawala bora, uwajibikaji wa kampuni na kiroho katika mfano mmoja wa fedha endelevu kulifanya mada hii iwe ya vitendo na yenye kutia motisha.

## Ghana na hatua kuelekea benki za Kiislamu

**Benki Kuu ya Ghana (Bank of Ghana) imekutana na wadau kujadili uwezekano wa kuanzisha mfumo wa benki wa Kiislamu nchini. Hii ni hatua nzuri, kwa kuwa inalenga kufafanua dhana potofu kuhusu maana halisi ya benki za Kiislamu.**

**Njia hii ya mashauriano inawapa Waghana wa dini zote nafasi ya kuangalia zaidi ya jina na kuuona benki wa Kiislamu kama mfumo wa kifedha wa kimaadili unaojengwa juu ya usawa, ustawi wa pamoja, na ujumuishaji wa kiuchumi.**

**Mikutano hii pia inaweka msingi muhimu kwa utekelezaji mzuri wa masharti ya "benki zisizo na riba" yaliyomo kwenye Sheria Na. 930, mara tu mifumo ya udhibiti na usimamizi itakapokamilika.**

### Mfumo wa benki wa Kiislamu ni nini?

**Mfumo wa benki wa Kiislamu (au benki isiyo na riba) ni mfumo mbadala wa fedha unaoongozwa na mgawanyo wa hatari, uzuiaji wa riba (riba), kuepuka kamari/ubashiri, na kuwekeza kwenye miradi yenye manufaa ya kijamii.**

**Ingawa unatokana na maadili ya Kiislamu, si ibada ya kidini kwa vitendo. Huhitaji kuwa Muislamu ili kutumia huduma hizi—kama tu mtu hahitaji kuwa Mkatholiki ili kupata huduma hospitalini ya Kikatholiki.**

### Kujibu wasiwasi wa wakosoaji

**Shaka kutoka kwa baadhi ya watu wa kidini inaeleweka kwa kuwa jamii ya Ghana ina utambulisho wa kidini ulio imara. Hata hivyo, mfumo wa benki wa Kiislamu haukusudiwi kutawala kidini.**

**Ni mfumo unaotanguliza maadili—ukilingana na kanuni nyingi za Ukristo kama haki, uadilifu, uangalizi wa rasilimali, na huruma kwa wasiojiweza. Ni mtindo wa biashara unaolenga maadili na kuwezesha kiuchumi, si chombo cha ubabe wa kidini.**

### Manufaa kwa uchumi wa Ghana

**Kuanzishwa kwa mfumo wa benki wa Kiislamu kunaweza kusaidia malengo mapana ya maendeleo ya uchumi. Kando na kutoa njia mbadala, kunaweza kuongeza ujumuishaji wa kifedha, kuvutia mtaji, na kuhimiza mazoea ya kifedha ya kimaadili na endelevu.**

**Inakadiriwa kuwa watu wazima 30–40% Ghana hawana huduma rasmi za kifedha. Baadhi yao hukataa benki za kawaida kwa sababu za maadili au imani kuhusu riba. Benki isiyo na riba inaweza kuwavuta kundi hili kwenye mfumo rasmi.**

**Wengi ambao maadili au imani zao hupinga riba wamelazimika kutumia benki za kawaida kinyume na dhamira zao. Mfumo wa benki wa Kiislamu unaweza kuoanisha imani zao na mienendo yao ya kifedha.**

**Ufadhili wa Kiislamu unaweza kuvutia mitaji ya kimataifa inayopendelea kugawana hatari na mikopo yenye dhamana halisi. Pia, benki za ndani zinaweza kupanua bidhaa—kutoa huduma zisizo na riba, kupunguza hatari ya kutegemea bidhaa chache, na kuimarisha uimara wa sekta.**

**Mbinu ya msingi-wa-mali na mgawanyo wa hatari inafaa sana kwa kilimo na biashara ndogo. Sekta hizi mara nyingi hukosa huduma na benki za kawaida kwa kuonekana kuwa na hatari kubwa, ilhali mfumo wa benki wa Kiislamu unaweza kutoa ubia na miundo inayowafaa.**

المؤسسة الإسلامية

The Islamic Foundation

# CHANGIA GAZA



yas | Mixx **0716 542 323**

**Jina: THE ISLAMIC FOUNDATION**

m-pesa **0768 111 877**

**Jina: THE ISLAMIC FOUNDATION**

CRDB BANK **0150657264700**

**Account: THE ISLAMIC FOUNDATION**

LIPA **15441517**

**Jina: THE ISLAMIC FOUNDATION**

airtel money **0696 568 625**

**Jina: THE ISLAMIC FOUNDATION**

# KUTOKA KWA MHARIRI

Msamvu, Morogoro
P.O.Box 6011
Morogoro,
Tanzania

Mhariri
+255 789 201383

# Hili la maharimu 'kuoana' daima lisifumbiwe macho

Hivi karibuni, Mahakama ya Wilaya ya Maswa mkoani Simiyu iliwahukumu kifungo cha miaka 20 na 30 jela ndugu wawili, Mussa Shija (33) na Hollo Shija (36) baada ya kukutwa na hatia ya kuzini na maharimu (kujamiiana na ndugu wa damu) na hatimaye kupata mtoto.

Hukumu hiyo ilitolewa Oktoba 6, 2025 na Hakimu Mkazi wa Mahakama hiyo, Aziz Khamis, ambaye alimhukumu Mussa Shija kutumikia kifungo cha miaka 20 jela huku dada yake, Hollo Shija akihukumiwa miaka 30.

Ndugu hao ambao ni watoto wa baba na mama mmoja walisomewa shtaka la kuzini na maharimu, ambalo ni kinyume na kifungu cha 158 (1) (b) na kifungu cha 160 cha Sheria ya kanuni ya adhabu sura ya 16, Marejeo ya Mwaka 2022.

Katika kesi hiyo ya jinai namba 10745 ya mwaka 2025, upande wa mashtaka uliwasilisha mashahidi 11 na vielelezo vitano, ikiwamo ripoti ya uchunguzi wa vinasaba (DNA) kutoka Ofisi ya Mkemia Mkuu wa Serikali iliyoonesha kwa asilimia 99.99 Mussa na Hollo ni watoto halali wa Shija Kamuga ambaye ndiye baba yao mzazi, na asilimia 99.99 ikionesha mtoto aliyezaliwa wakati wanaishi kama mke na mume ni mtoto wao.

Hata hivyo, washatkiwa wote wawili walikana shtaka hilo wakidai kuwa Shija Kamuga si baba yao mzazi bali ni jirani yao tu na alifungua kesi hiyo kwa sababu ya wivu na chuki binafsi.

Sisi, kama chombo cha habari cha Kiislamu tumefurahishwa na uamuzi wa Mahakama wa kuwafunga gerezani ndugu hao wawili, kwani kitendo walichofanya si tu ni kinyume na maelekezo ya dini bali ni kitendo cha aibu na kinachokiuka Katiba, sheria na mwongozo wa maadili ya Mtanzania na Afrika kwa ujumla.

Maharimu wanapotenda kosa la uzinifu, tafsiri yake ni kuwa wametumia uhuru wao vibaya hivyo wanastahili adhabu kwa mujibu wa sheria ili iwe fundisho kwao na onyo kwa wengine wenye nia au lengo la kufanya uovu huo.

Uislamu unakataza kufunga ndoa na ndugu wa damu au wale ambao ni haramu kuwaoa, kama anavyobainisha Mwenyezi Mungu: "Mmeharamishiwa (kuwaoa) mama zenu, na mabinti zenu, na dada zenu, na shangazi zenu, na makhalati zenu (mama wakubwa na wadogo), na mabinti wa kaka (zenu), na mabinti wa dada (zenu), na mama zenu ambao wamekunyonyesheni, na dada zenu kwa kunyonya, na mama wa wake zenu, na watoto wenu wa kambo walio katika ulinzi wenu waliozaliwa na wake zenu ambao mmewaingilia. Lakini ikiwa hamkuwaingilia basi hakuna dhambi (kuwaoa)..." [Qur'an, 4:23].

Kadhalika, Sheria ya Ndoa Tanzania inakataza mtu kuoa au kuolewa na mzazi wake, mzazi wa mzazi wake, mtoto au mjukuu wake, kaka au dada yake, mama au shangazi yake, au baba wa mjomba wake.

Wengine ambao wamo kwenye kundi la maharimu (usioweza kuwaoa) ni mama wa kambo na mtoto uliyemuasili (adoption). Kisheria ni kosa la jinai kwa mtu kujamiiana na maharimu wake (achilia mbali kumuoa/ kuolewa nae) hata kama wote wawili walikubaliana kufanya kitendo hicho.

Kwa sababu ya kulinda maslahi mapana ya jamii na Taifa, tunashauri itungwe sheria kali itakayowabana watu wengine wanaojihusisha na vitendo vya zinaa. Sambamba na hilo, tunapenda kwa nia njema kabisa kutoa wito kwa mamlaka husika kuchukua hatua kudhibiti vichocheo vya zinaa kama vile madanguro, ulevi, kumbi za starehe, na wanawake kuvaa nguo fupi, zinazobana, au zinazoonesha maungo ya mwili.

Msisitizo hapa ni kawmba, ili kukabiliana na madhara ya muda mrefu ya zinaa, ni wajibu wetu kama jamii kuzishika na kuziishi amri za Mwenyezi Mungu ikiwa ni pamoja na kujitenga na madhambi ya zinaa na uasherati, ambayo Mwenyezi Mungu ameyataja katika Qur'an kama uchafu mkubwa na njia mbaya, [Taz: 'Qur'an, 17:32'].

ربيع ثان

# HABARI KIMATAIFA

MAHMOUD NYAMGUMA



# Faraja kwa wapenda haki wakati Israel ikijiondoa Gaza

Jeshi la Israel limeanza kujiondoa baadhi ya maeneo ya Ukanda wa Gaza chini ya hatua ya kwanza ya makubaliano ya kusitisha mapigano yaliyopatanishwa na Marekani.

Vyombo vikuu vya habari vimethibitisha kuanza kwa usitishwaji mapigano na kurudi kwa raia kwenye maeneo yao, pamoja na kuanza kwa uondoaji wa wanajeshi katika baadhi ya maeneo na matarajio ya ongezeko la malori ya misaada.

Hata hivyo, utaratibu wa utekelezaji bado una maswali mengi kuhusu usimamizi wa Gaza baada ya vita na kasi ya kuingia kwa misaada

Maelfu ya Wapalestina wanaorejea wanakuta makazi yao yakiwa magofu baada ya vita vya zaidi ya miaka miwili. Vifo vinadaiwa kuvuka 67,000, kwa takwimu za mamlaka za afya za Palestina zilizoripotiwa na vyombo vya kimataifa.

UNRWA imesema ina uwezo wa kuingiza msaada sawa na malori 6,000 ya vyakula na dawa endapo vizuizi vitaondolewa. WFP na UNICEF wameonya vifo vya watoto vinaweza kuongezeka ikiwa mtiririko kamili wa misaada hautaruhusiwa, huku mpango wa kusitisha mapigano ukitarajiwa kuruhusu mamia ya malori kila siku.

Wizara ya Afya ya Gaza imeripoti kuwa zaidi ya wahudumu wa afya 1,700 wameuawa tangu 2023, hospitali nyingi zikiwa bila dawa, umeme na maji; ripoti za haki za binadamu zinaeleza zaidi ya asilimia 70 ya miundombinu ya afya imeharibika vibaya, ikielekeza uwezekano wa uhalifu wa kivita.

Mashirika na viongozi wa Kiislamu wametaka utekelezaji wa haki wa makubaliano hayo, wakionya usalama wa Wapalestina hauwezi kupatikana kwa kuvunja utu wao. Waziri wa Mambo ya Nje wa Uturuki Hakan Fidan ameonya uchokozi wowote unaweza kuvuruga utulivu. Maandamano ya kuunga mkono amani na Wapalestina yameonekana katika miji mbalimbali duniani.

Licha ya makubaliano, Israel inaendelea kushikilia miili ya Wapalestina waliouawa, jambo linaloongeza maumivu kwa familia. Viongozi wa Hamas na makundi mengine wamesema hawatakubali udhibiti wa kigeni juu ya Gaza na wanapendekeza mkutano wa kitaifa wa ujenzi wa umoja na mkakati wa ujenzi upya.

Wachambuzi wanaonya uwezekano wa Israel kuendelea kuhalalisha uwepo wa kijeshi kwa hoja ya "tishio la kiusalama," hali ambayo inaweza kuhatarisha amani ya muda mrefu.

Wito kwa uchunguzi huru wa ICC kuhusu ukiukaji mkubwa wa haki za binadamu unaendelea; pia kuna taratibu zinazoendelea katika ICJ na uchunguzi wa Mwendesha Mashtaka wa ICC kuhusu uhalifu unaodaiwa kufanywa na pande zote katika eneo la Palestina.


ربيع ثان

MAKALA MAALUM

NA SHEIKH SEIF RUGA



# Wajue wanawake walio haramu kuwaoa




Uislamu umehalalisha ndoa kwa wanawake, lakini umekataza ndoa kwa baadhi yao kwa hekima kubwa. Moja ya hekima hizo ni kwamba, uhusiano wa karibu wa kifamilia (maharimu) una nguvu ya kudumu, hivyo hauhitaji tena kuimarishwa kupitia ndoa.

Kuna heshima maalumu inayopaswa kuzingatiwa baina ya maharimu, ambayo inaweza kugongana na haki na wajibu wa ndoa. Kwa hivyo, kulinda mipaka hiyo ni jambo la lazima na la muhimu. Walioharamishwa kuwaoa katika Uilsmu wapo aina mbili; kuna walioharamishwa kuwaoa milele na wengine kwa muda mfupi.

Katika makala haya tutaangazia wanawake ambao ni haramu kuwaoa milele, kwa maana ya maharimu. Wanawake wa aina hii, sharia imehalalisha kusafiri nao, kukaa nao faragha, kuwatazama, na kusalimiana nao kwa kushikana mikono.

Iwapo mtu atamuoa mmoja wa wanawake hawa huku akijua wazi kuwa ni haramu kumuoa, basi atahukumiwa adhabu ya kifo. Hilo limethibiti katika dini kutokana na yale yaliyopokewa kwa Mtume (rehema na amani ziwe juu yake) kwamba, siku moja aliamuru kuuawa kwa mtu mmoja aliyefunga ndoa na mwanamke aliyewahi kuolewa na baba yake, baada ya kufahamishwa juu ya uharamu huo, ***[Ahmad]***.

Imekatazwa kuoa mwanamke aliye maharimu kwa sababu kubwa nne ambazo ni undugu (qaraaba), ukwe (musaahara), kunyonya ziwa moja, na kulaaniana (li'aan).

Walioharamishwa kuwaoa kwa sababu ya undugu wapo aina nne. Kwanza ni mama mzazi na bibi (na wote wanaowafuata kwenda juu katika kizazi) – iwe bibi wa upande wa baba au mama. Allah anasema: "Mmeharamishiwa (kuwaoa) mama zenu." ***[Qur'an, 4:23]***.

Pili, watoto na wajukuu wa kike (na wote wanaowafuata kwenda chini katika kizazi), pamoja na binti aliyezaliwa kwa njia ya zinaa, au kwa mume aliyemlaani mkewe.

Tatu, dada wa tumbo moja au aliyetokana na baba mmoja au mama mmoja, mabinti wa dada na kaka (na wanaowafuata kwenda chini katika kizazi). "Mmeharamishiwa (kuwaoa) mama zenu, na mabinti zenu, na dada zenu, na shangazi zenu, na mama zenu wadogo, na mabinti wa kaka na mabinti wa dada." ***[Qur'an, 4:23]***.

Hii inajumuisha pia dada aliyezaliwa kwa njia ya zinaa, mabinti wa kaka au dada waliozaliwa kwa njia ya zinaa, na wote wanaotokana na vizazi vyao.

Nne, shangazi (dada wa baba), mama wadogo au wakubwa, pamoja na mama zake wadogo baba na mama, na pia mama zake wadogo babu na bibi wa juu katika familia. Vilevile, ni haramu mwanamke kuolewa na mjomba wake, ami yake (baba mkubwa au mdogo), mjomba wa baba yake au mama yake, na baba mkubwa au mdogo wa baba yake au mama yake.

## Walio haramu kuwaoa kwa sababu ya ukwe

Wanawake walioharamishwa kuwaoa kwa sababu ya ukwe (muṣaahara) wapo aina nne. Kwanza, wazazi wa mke. Hawa ni pamoja na mama wa mke na bibi zake wote wa upande wa baba na mama. Uharamu huu ni baada ya ndoa tu kufungwa, bila kujali kama mume amefanya tendo la ndoa na mke au la.

Pili, mabinti wa mke na wajukuu zake wote. Hawa uharamu wao unathibiti ikiwa mume amefanya tendo la ndoa na mke (mama yao). Ikiwa ndoa imefungwa lakini tendo la ndoa halikufanywa hawaharamiki, kwa neno lake Mwenyezi Mungu Mtukufu: "....na watoto wenu wa kambo walio katika ulinzi wenu waliozaliwa na wake zenu ambao mmewaingilia. Ikiwa hamkuwaingilia basi hapana lawama juu yenu." ***[Qur'an, 4:23]***.

Pia, binti wa mtoto wa kiume wa kambo anaingia katika hukumu (sharia) hii. Kanuni ya kisheria inasema: "Kufunga ndoa na binti kunamharamisha mama, na kumuingilia mama kunamharamisha binti."

Tatu, wake wote wa baba na babu upande wa baba au mama. Hawa uharamu wao unathibiti kwa kufunga ndoa, hata kabla ya kuwaingilia. Allah anasema: "Wala msiwaoe wanawake walioolewa na baba zenu, isipokuwa yaliyokwishapita (huko nyuma)." ***[Qur'an, 4:22]***.

Nne, wake wa watoto au wajukuu wa watoto wa kiume au wa kike, hata kama tendo la ndoa halikufanyika. "(Na mmeharamishiwa) wake wa watoto wenu waliotoka kwenye migongo yenu..." ***[Qur'an, 4:23]***.

## Walio haramu kuwaoa kwa sababu ya kunyonya pamoja

Kunyonya ziwa moja (Ar–Radha) kunafanya watoto wawe na uhusiano sawa na ule wa damu kati ya mtoto aliyenyonyeshwa, na familia ya mama aliyemnyonyesha. Hivyo basi, mama wa kunyonyesha anachukua nafasi ya mama wa asili, na mume wa mama aliyenyonyesha anachukua nafasi ya baba wa asili, vivyo hivyo kwa ndugu zake wengine wa upande wa mama aliyenyonyesha. Uharamu wao unatokana na kunyonya pamoja.




SEHEMU YA 1

MUSSA IMANI
SHEHA,
ZANZIBAR
0773 181 494



# HUDHAYFA BIN AL-YAMAN: Mtunza Siri za Mtume

## VISA VYA MITUME NA MASWAHABA

## Jina na nasabu yake

Jina lake ni Hudhayfa bin al-yaman bin Jabir bin Harith al-Absy. Ni mmoja wa Maswahaba mashuhuri wa Mtume (rehema za Allah naa amani zimshukie), mbobezi katika fani za fiqhi, tafsiri na tarbiya; mpiganaji shujaa, mchamungu na aliyejipamba kwa tabia njema. Mama yake ni Rababa bint Ka'b bin 'Ady. [Al-Isaba 4:300]. Hudhayfa alizaliwa Makka na akakulia Yathrib (Madina). Inaelezwa kwamba baba wa Hudhayfa, mzee Al-yaman, ni mtu wa Makka, lakini zamani alikimbilia Yathrib baada ya tukio la kumuua mtu. Wenyeji wake huko ni kabila la al-Ashhal. Alimuoa Lubaba na kupata mtoto Hudhayfa. Ulipokuja Uislamu, wazazi wa Hudhayfa walikuwa miongoni mwa wa mwanzo-mwanzo kusilimu. Kwa hali hiyo, Hudhayfa akakulia katika nyumba (familia) ya Kiislamu na kupata malezi ya wazazi wake; nyumba iliyojaa nuru ya imani, matendo mema na uchamungu.

### Hudhayfa kukutana na Mtume

Shauku ya Hudhayfa ya kumuona Mtume (rehema za Allah na amani zimshukie) ilikuwa haielezeki tangu aliposikia habari zake, na akimuulizia kila siku.

Hatimaye alisafiri kuelekea Makka. Alipokutana naye tu, alimuuliza: "Mimi ni katika Muhajirina au ni katika Answar?" Mtume akamwambia: "Upendavyo; ukipenda kuwa katika Muhajirina sawa, au kuwa katika Answar hakuna shida, chagua mwenyewe." Hudhayfa akasema: "Basi mimi ni katika Answar."

### Mahusiano ya Hudhayfa na Mtume Madina

Hazikupita siku nyingi Mtume alihamia Madina. Hudhayfa alimlazimu Mtume (alijiweka pamoja naye) kama pete na kidole, na alishiriki pamoja naye vita vyote, ukitoa Badr.

Tumnukuu mwenyewe anajieleza: "Hakuna kilichonizuia kwenda vita vya Badr isipokuwa kwamba mimi na baba yangu tulikuwa nje ya Madina; tulishikwa na makafiri wa Kikureishi wakatuuliza: 'Mnakwenda wapi?' Tukasema: 'Madina.' 'Mnakwenda kumsaidia Muhammad?' Tukasema: 'Hapana, tunakwenda tu Madina.' Hawakutuachia mpaka wakachukua ahadi zetu za kutomsaidia Mtume, kisha wakatuachia. Tulipofika Madina tulimueleza Mtume yaliyotukuta na kumuuliza tufanye nini? Akasema: 'Timizeni ahadi, tumtegemee Allah na tujilinde na shari zao.'" Kwa hiyo tukabaki Madina.

### Hudhayfa katika vita vya Uhud

Ilipofika siku ya vita vya Uhud, Hudhayfa alitoka pamoja na baba yake. Huku akiwa katika nyota za vita hivyo, baba yake, mzee Al-yaman, aliuliwa na Waislamu wenzake kimakosa.

Mkasa wenyewe ulikuwa kama hivi: katika vita hivyo, Mtume (rehema za Allah na amani zimshukie) aliwaweka Al-yaman na mzee mwenzake Thabit bin Qays pamoja katika hifadhi ya wanawake.

Vita ilipopamba moto, Al-yaman alimwambia mwenzake: "Tunasubiri kitu gani hapa ilhali haukubakia umri wa mmoja wetu ila kiasi cha punda kunywa na kushiba maji? Sisi ni maiti wa leo au kesho! Basi kwa nini hatushiki panga zetu na kwenda kuungana na Mtume wa Allah, huenda Allah ataturuzuku Shahada (kufa mashahidi) tukiwa na Mtume wake." Wakachukua panga zao wakaingia katika kundi la watu (wapiganaji).

Mzee Qays akauliwa na makafiri; ama Al-yaman, baba wa Hudhayfa, alishambuliwa na panga za Waislamu wasiomjua, wakidhani ni miongoni mwa maadui, huku mwanawe Hudhayfa akinadi: "Jamani, baba yangu! Jamani, baba yangu!" Hakuna anayesikia (anayeelewa) mpaka akaanguka chini maiti.

Hudhayfa akawa anasema: "Allah akusameheni." Mtume alitaka kumlipa diya, lakini Hudhayfa alikataa akisema: "Inaniliwaza kwamba baba alitoka kuitafuta Shahada na amefanikiwa kuipata; ewe Allah, shuhudia kwamba diya ya baba yangu nimeitoa sadaka kwa Waislamu."

Tukio hili lilimuongezea Hudhayfa nafasi kubwa mbele ya Mtume (rehema za Allah naa amani zimshukie). [Taz. Suwarun min Hayat Sahaba, uk. 299–300]



# MAPITIO YA KITABU

NA UKHTI FATIMA SS

**JINA LA KITABU:** TOFAUTI YA KUSHAURI NA KUABISHA
**MTUNZI:** AL-HAAFIZ IBN RAJAB AL-HANBALI

## Utangulizi wa kitabu

Kitabu hiki kifupi lakini chenye uzito kimeandikwa na Al-Ḥāfiẓ Ibn Rajab Al-Hanbali (736–795 H), mfuasi mashuhuri wa madhehebu ya Hanbali na miongoni mwa mahafidh waliobobea katika fani ya hadith na fiqhi ya tabia huku pia akisifiwa kama mtafiti huru anayejenga hukumu juu ya dalili.

Toleo linalopatikana la kitabu hiki leo limetolewa na Dar As-Sunnah Publishers, na limeongezewa maelezo yenye manufaa ya Dkt Ṣāliḥ ibn Sa'd al-Suṣaymi ili kulifanya liwe na uhalisia katika muktadha wa karne hii.

Kama kichwa chake kinavyoashiria, kazi hii inachambua tofauti nyeti kati ya nasaha (ushauri mwema) na kukejeli/kuaibisha. Hili ni eneo ambalo mara nyingi huchanganywa hata na watu wema, hasa tunapokabiliana na hitilafu za maoni ndani ya Ahl as-Sunnah.

Ibn Rajab anapanga misingi, adabu na mipaka ya ukosoaji, akisisitiza kwamba kanuni hizi zimetungwa kwa ajili ya Watu wa Sunnah—wanaotafuta haki, rehema na islah—si kwa wafuasi wa bid'ah na matamanio.

## Kwa nini kitabu hiki ni muhimu?

Kwanza, kinatoa miongozo ya kiusuli na kiadabu kwa wale wanaofanya da'wah, kufundisha au kuandika mihadhara na makala. Katika zama za mitandao ya kijamii ambako "ukosoaji" mara nyingi hugeuka kejeli hadharani, maandishi haya ni dira inayotenganisha baina ya kujenga na kubomoa.

Pili, kitabu hiki kinarejesha mjadala kwenye mizani ya Shariah: kipi ni faradhi ya kuamrisha mema na kukataza maovu, na kipi ni kupitiliza mipaka kwa lugha, nia na mbinu.

Tatu, kitabu kinawasaidia wanafunzi wa elimu ya Kiislamu, wahariri na waandishi wa habari wa Kiislamu kutofautisha baina ya ukweli unaolenga islah na uungwana unaolinda heshima ya Muumini—ikiwa ni sehemu ya kujenga jamii yenye nidhamu ya mazungumzo.

Pia, mchango wa Dkt. Al-Suṣaymi katika sherehe zake unafanya fikra za Ibn Rajab ziende mbali zaidi ya nadharia: anazifungamanisha na mazingira ya sasa—mikutano, mijadala ya kifiqhi, mihadhara ya mtandaoni, hadi namna ya kuandika radd bila kusababisha fitna.

## Nukta muhimu za mafundisho ya kitabu hiki

Mosi, nia ndiyo kiini: nasaha dhidi ya kuabisha/kukejeli. Ibn Rajab anasisitiza kuwa nasaha inalenga kumrejesha ndugu kwenye haki kwa upole, ikitafuta radhi za Allah na manufaa ya mshauriwa. Kejeli/kuabisha kunalenga kudhalilisha, kujionyesha au kulipiza kisasi; hata ikiwa maneno ni ya kweli, nia ovu huiharibu.

Pili, fuata njia zilizo halali na zenye mizania. Ushauri unapaswa kufanywa kulingana na hali, kwanza, ya anayoshauriwa (uelewa, unyeti, hadhi); uhusiano kati ya mshauri na mshauri wa (ukaribu huongeza uwezekano wa kukubaliwa); uovu uko wazi au siri? (siri hushughulikiwa kwa faragha; ya wazi hurekebishwa kwa hekima hadharani). Jambo jingine la kuzingatiwa ni je madhara ya kosa, kwa maana, yanamrudia mkosaji peke yake au yanawaathiri wengi?

Tatu, kutaja kosa si vibaya bali ipimwe kwa mzani wa nia na mtindo. Mara nyingine, kueleza kosa au kutaja udhaifu wa mtu ni sehemu ya nasaha, ilimradi lengo si kumtia aibu bali kumuongoza. Kinyume chake, kutumia kosa lake kama jukwaa la kujipandisha hadhi ni kejeli na kuabisha kulikokatazwa.

Nne, mipaka ya ukemeaji na hukumu kali. Kumuita mtu kafiri au asi kuna mipaka na masharti. Haifanywi kwa pupa wala bila ushahidi. Hii inalinda haki ya mtu na heshima ya jamii, na kuzuia mgawanyiko usio wa lazima.

Tano, kanuni hizi ni mahsusi kwa Ahl as-Sunnah. Kwa wanaojulikana kwa kufuata haki na kuonyesha rehema, nasaha inatangulia, majadiliano yanafanywa kwa hoja na uthibitisho, na lengo ni matengenezo ya watu na kujua ukweli. Kwa wafuasi wa bid'ah, mbinu hubadilika kwa mujibu wa maslahi ya Shariah na madhara yanayozingatiwa.

Sita, ukosoaji unaojenga: misingi sita ya kiutendaji. Kwanza, tathmini madhara/maunfaa kabla ya kuzungumza; pili, chagua mahali na wakati ufaao ikiwezekana penye faragha ni bora. Tumia lugha yenye haki: sahihi, fupi, isiyo ya kejeli. Onesha njia mbadala na hatua za kurekebisha, sio kosa tu lakini pia epusha ujumuishaji: kosoa kitendo, si kuharibu utu mzima. Muhimu zaidi, jikague: jiulize kama unachochewa na nafsi au kwa ajili ya Allah.

Saba, epuka kuwasha moto mitandaoni. Katika Facebook, X au majukwaa ya mihadhara, nasaha ya kweli huepuka "kuwasha moto". Ukosoaji wa kisomi unahitaji vyanzo, muktadha na uadilifu wa kunukuu. Tujue kuwa taharir ya Kiislamu yahifadhi sitara na udugu hata inapokosoa.

Nane, jukumu la moyo na maadili binafsi. Mtu anayenasihi anapaswa kuwa na taqwa, huruma na subira. Mara nyingi, sauti na sura ya ushauri ndiyo hupokelewa kabla ya yaliyomo.

ربيع ثان

NASAHA ZA WIKI



NA YUSUFU AMINI
0787 503 085

# Maisha yetu katika dunia iliyoharibika

Katika miaka ya sasa kumekuwa na wimbi kubwa la vitendo viovu vinavyokiuka maadili ya dini. Ukiiangalia dunia hivi sasa, utabaini hakuna hata bara moja lisilo na changamoto ya mmomonyoko wa maadili.

Hii inatokana na kile kinachojulikana kwamba, kheri na shari ndiyo msingi mkuu wa tabia zote zinazotawala maisha ya binadamu hapa ulimwenguni. Mwenyezi Mungu anasema: "Na tunakujaribuni kwa mtihani wa shari na kheri. Na kwetu Sisi mtarejeshwa." [Qur'an, 21:35].

Kwa sababu ya kuwapo vitendo vya kheri na shari hapa ulimwenguni, Uislamu umewaamirisha wafuasi wake kuwajibika katika kuamrishana mema na kukatazana maovu. Mtume (rehema za Allah na amani iwe juu yake) ametuambia, Allah ni Mzuri na hakubali isipokuwa mazuri.

Kwa hiyo tunapaswa kuyapima matendo yetu kwa jinsi yatakavyotupa faida au kutujengea hadhi mbele ya Mwenyezi Mungu. Isivyo bahati tulio wengi tumepoteza mizani hii, na badala yake tumezama katika kupima mambo kwa vipimo vya kidunia zaidi pasina kujali kutafuta radhi za Mwenyezi Mungu.

Hali hii inakwenda kinyume na malengo ya Muumini, ambaye siku zote anapaswa kujipima kupitia matendo yake – yawe ya shari au ya kheri. Muumini hupima matendo yake kwa kuangalia je, nikifanya kitendo hiki nitapata radhi za Mwenyezi Mungu au nitamkasirisha?

## Mtazamo wa wanafalsafa kuhusu maovu

Wanafalsafa wa kale wa Kimagharibi na wasomi wa elimu ya Theologia wamejaribu kuelezea vitendo viovu kwa kutumia maarifa yao. Mfano, mwanafalsafa wa Kigiriki aitwaye Socrates amefundisha kuwa, kwa vile maadili ni matokeo ya elimu, basi maovu au dhambi ni matokeo ya ujinga.

Socrates anasema, mtu ambaye alikuwa anajihusisha na madhambi ilihali anajua, huyo ni mjinga. Maana yake ni kwamba, binadamu kama kiumbe mwenye akili hapa ulimwenguni, kazi yake kubwa ni kuongoza maisha yake kwa kuwa yeye ni kiumbe mwenye tabia ya kufikiri.

Mwanafalsafa mwingine anayejulikana kwa jina la Plato amesema, asili ya maovu hapa duniani ni kwamba, ndani ya roho ya mtu kuna maumbile yenye uwezekano wa kuwepo kwa mvurugano (disorder) unaopelekea kuwapo kwa maovu au dhambi.

Plato anaendelea kusema, mvurugano hutokea kwenye roho ya binadamu hivyo chanzo cha uovu lazima kitafutwe kwenye roho, kwani maovu au dhambi ni usahaulifu na ujinga ambao hutokea ndani ya roho yenyewe juu ya dira ya ukweli.

Ukifuatilia maelezo ya wanafalsafa hawa, utaona kuwa chanzo cha maovu yote ni wanadamu wenyewe. Watu wanapokataa kumuabudu na kumtii Mwenyezi Mungu hutumbukia kwenye maovu kutokana na kufuata ushauri wa Iblis. Maovu kama wizi, ulevi, uzinzi, kucheza kamari, kuwaua watu wasio na hatia, kuvunja mkataba au makubaliano – ni matokeo ya wanadamu kutumia vibaya uhuru waliopewa na Allah na kutotimiza wajibu wao kama binadamu.

Sote tunajua kuwa duniani kuna vizuri na vibaya, lakini vibaya ni vingi na vinapendeza zaidi katika macho ya wanadamu. Mwenyezi Mungu anasema: "Hawawi sawa wabaya na wema, hata huo wingi wa wabaya ukikufurahisha (usimili katika wingi huo). Basi mcheni Mwenyezi Mungu enyi wenye akili ili mpate kufanikiwa." [Qur'an, 5:100].



Katika taratibu (Sunan) za Mwenyezi Mungu katika ulimwengu huu, ni kuwapo uongofu na wema, haki na batili, kunyooka sawasawa na kupondoka – lakini vyovyote iwavyo, ukweli utabakia siku zote kwamba Qur'an ndiyo kipimo cha haki na uadilifu.

Mwenyezi Mungu ametubainishia wazi kuwa Waumini hawalingani na waovu, si katika matendo wala malipo: "Ati aliye Muumini atakuwa sawa na aliye mpotovu? Hawawi sawa. Ama walioamini na wakatenda mema, watakuwa katika bustani za makazi mazuri, ndiyo pa kufikia kwa waliyokuwa wakiyatenda. Ama wale waliotenda uovu, basi makazi yao ni motoni. Kila wakitaka kutoka humo watarudishwa humo humo. Na wataambiwa, 'Onjeni adhabu ya moto mliyokuwa mkiikanusha.'" [Qur'an, 32:18–20].

Kama ambavyo hawatalingana katika maisha ya Akhera, vilevile watu wema na waovu hawalingani katika maisha haya ya dunia. Mwenyezi Mungu anahoji: "Je! Wanadhani wanaotenda maovu kuwa tutawafanya kama walioamini na wakatenda mema, sawasawa katika uhai wao na kufa kwao? Ni hukumu mbaya wanayoihukumu!" [Qur'an, 45:21].

Sasa kwa kuwa maasi yamekuwa mengi hivi sasa, tuna wajibu, jukumu na dhima ya kukemea kadiri ya uwezo wetu yale yote ambayo Mwenyezi Mungu na Mtume wake wameyakataza, kama tulivyoamriwa katika hadith: "Atakayeona uovu auondoe kwa mkono wake, na asipoweza (auondoe) kwa ulimi wake, na akishindwa achukie moyoni – na huo ni udhaifu wa imani." [Muslim].

Kwa kuzingatia kauli hii ya Mtume, kila mmoja wetu anatakiwa akerwe na maovu na kuyapiga vita, kwani madhara yanapojitokeza huwakumba wanaohusika na wasiohusika. Historia inaonesha kuwa katika kila zama hapakosekani kundi kubwa la watu ambao dhamira yao ni kufanya uharibifu katika ardhi kwa maslahi yao binafsi.

Kwa sababu ya kutenda kwao maovu, dunia imekuwa ikikabiliwa na matatizo na majanga mbalimbali huku kukiwa na kikundi kidogo tu cha watu kinachokataza na kuzuia uovu huo. Waharibifu wanaposhamiri na maovu kuenea, mvutano huwa ni mkubwa kwa sababu lengo la waharibifu ni kutoboa jahazi ili wasalimike hata kama watu wengine wataangamia.

JUNAYNAT ALLY DAMA

# Utafiti: Mwenye saratani akiacha tumbaku huongeza umri wa kuishi mara mbili zaidi



Wazo kwamba "umeshachelewa" kuacha kuvuta sigara baada ya utambuzi wa saratani limekuwa likijirudia katika mazungumzo ya wagonjwa na hata katika baadhi ya vyumba vya tiba.

Hata hivyo, utafiti mpya ulioripotiwa na Medscape unalipindua vikali wazo hilo: miongoni mwa wagonjwa 13,282 waliotibiwa katika kliniki za saratani, wale walioacha kuvuta sigara ndani ya miezi sita tangu ziara yao ya kwanza walionesha uhai wa karibu mara mbili ukilinganishwa na wale waliodumu kuvuta sigara.

Ingawa ni 22.1% tu ya wavutaji wa sasa walioweza kuacha, faida ya kuishi ilikuwa dhahiri katika hatua zote za saratani, ikionesha kwamba kuacha ni tendo lenye thamani hata unapochelewa kuanza nalo.

Chanzo cha taarifa hizi ni uchunguzi wa kundi la wagonjwa waliotembelea kliniki kati ya Juni na Desemba 2018, kisha kufuatiliwa kwa miezi sita mbele ili kuthibitisha kama wameacha au la.

Watafiti walitumia mbinu za takwimu kupima uhai wa miaka miwili kwa kuzingatia hali ya uvutaji katika ziara ya mwanzo na hatima ya kuacha ndani ya miezi sita. Kilichojitokeza ni taswira inayoeleweka kitaalamu: uvutaji unaendelea kuwa kizidishi kikubwa cha vifo, wakati kuacha—hata baada ya utambuzi—kunageuza mwelekeo wa hatima ya mgonjwa.

Kwa wenye saratani zilizo katika hatua za juu (III/IV), kudumu katika kuvuta sigara kuliongeza hatari maradufu. Makadirio ya uhai wa miaka miwili, baada ya kurekebisha sababu nyingine, yalionekana kuwa juu zaidi kwa wale wasiovuta kabisa (81.4%), yakifuatiwa na waliowahi kuvuta (79.4%), na kuwa chini zaidi kwa wavutaji wa sasa (76.4%). Kwa lugha nyepesi: kila hatua inayoelekea kuacha huongeza nafasi ya kuishi, na kuendelea kunapunguza.

Utafiti huu unaibua pia swali la kimfumo: je, madaktari hutia mkazo wa kusitisha uvutaji kwa wagonjwa wote kwa usawa? Ushahidi unaashiria kuwa msaada wa kuacha hutolewa kwa uchache kwa wagonjwa walio na saratani za hatua ya juu, mara nyingi kwa dhana potofu kwamba hakuna faida kubwa ya kitabibu katika wakati huo. Matokeo haya yanapingana na dhana hiyo na kupendekeza kubadili mazoea: kusaidia kuacha sigara ni sehemu ya tiba yenyewe, si nyongeza ya hiari. Waandishi wanasisitiza kwamba msaada wa kuacha uvutaji unatakiwa kutolewa kwa kila aliyenusurika saratani anayetumia tumbaku, bila kujali aina au hatua ya ugonjwa. Medscape

Ni muhimu pia kutazama mipaka ya utafiti huu kwa umakini. Hali ya uvutaji haikuthibitishwa kwa vipimo vya kibaolojia, hivyo uwezekano wa kuwepo kwa mgongano wa uainishaji. Aidha, faida iliyoonekana ya kuishi inaweza kuwa imechanganywa kwa sehemu na vipengele vingine vya afya—kama nidhamu kubwa ya kufuata tiba, mienendo mingine bora ya maisha.

Hata hivyo, kwa ukubwa wa kundi na uchanganuzi makini, ujumbe wa msingi unabaki kuwa: kuacha sigara kunaweza kubadilisha mwelekeo wa maisha baada ya saratani. Kwa wagonjwa, familia na watoa huduma, hoja hii ina tafsiri ya vitendo.

Kwanza, mazungumzo ya kuacha sigara yanapaswa kuanza siku ya kwanza ya tiba na kuendelea katika kila ziara—si kuacha baada ya "hali kutulia." Pili, timu ya saratani inapaswa kuunganisha programu za kusitisha uvutaji ndani ya utaratibu wa kawaida: ushauri wa tabia, tiba mbadala ya nikotini au dawa stahiki, na ufuatiliaji wa karibu wa miezi ya kwanza ambayo ndiyo hatari zaidi ya kurudi kwenye moshi.

Tatu, lugha nzuri ya huruma na kujali (sio lawama) na mtazamo wa mgonjwa (akusudie kutoka moyoni) ni muhimu katika kuleta mafanikio ya mgonjwa kuacha kuvuta tumbaku. Hata hivyo, kuondoa vizuizi vya upatikanaji wa huduma (gharama, muda, usafiri) huongeza uwezekano wa mafanikio.

Kwa watunga sera na wasimamizi wa huduma za saratani, takwimu hizi zinashauri maboresho ya mfumo ikiwa ni pamoja na kuhakikisha kila mgonjwa, ikiwemo aliye katika hatua ya juu, anapewa njia ya kutoka kwenye utegemezi wa tumbaku.

Kwa utafiti huu, ujumbe kwa jamii ni mwepesi lakini wenye uzito: kuacha sigara ni uwekezaji wa moja kwa moja katika muda wa kuishi, sio tu kwa wagonjwa wa saratani bali watu wote. Kila sigara isiyovutwa baada ya utambuzi ni hatua ndogo kuelekea siku nyingine ya kuishi.

ربيع ثان

MATUKIO YENYE MAZINGATIO

NA ZAHARANI BARAKA

# Sikiliza mahitaji yao na uwape kwa wema

Sa'ad bin Abi Waqqas (Allah amridhie) amesema, siku moja alimtembelea Abu Raafi'i, ambaye ni jirani yake na kukuta ana matatizo yaliyopelekea kuuza nyumba yake. Abu Raafi'i akamwambia Sa'ad: "Ewe Sa'ad, nunua nyumba yangu iliyopo katika mji wako." Sa'ad akasema: "Wallahi sinunui." Abu Raafi'i (Allah amridhie) akasema: "Wallahi utanunua." Sa'ad akamwambia Abu Raafi'i: "Sikupi zaidi ya dinari elfu nne na nitakulipa kwa awamu (kidogo kidogo)." Abu Raafi'i akasema: "Nimemsikia Mtume (rehema za Allah na amani zimshukie) akisema kuwa, jirani ndiye mwenye haki zaidi kwa kilicho karibu yake. Na kama Mtume asingesema hivyo nisingekuuzia nyumba yangu kwa dinari elfu nne kwa sababu nimeshapokea dinari elfu tano (kutoka kwa mnunuzi mwingine). Hatimaye Abu Raafi'I alimuuzia Sa' ad nyumba yake kwa dinari elfu nne." [Bukhari].

## Mafundisho ya tukio

Tukio hili linaonesha namna Masahaba (Allah awaridhie wote) walivyokuwa wakizingatia mafundisho ya Mtume (rehema za Allah na amani zimshukie) hata katika mambo yenye maslahi madogo ya kidunia. Abu Raafi'i aliacha kuuza nyumba yake kwa mtu ambaye alikuwa tayari kutoa dinari elfu tano, akamuuzia Sa'ad bin Abi Waqqas kwa dinari elfu nne kutokana na usia wa Mtume (rehema za Allah na amani zimshukie).

## Ujirani katika biashara

Tukio hili linaonesha umuhimu wa kuchunga na kusimamia haki za jirani hasa katika biashara zinazojumuisha mali zisizohamishika. Abu Raafi'i aliamua kuuza nyumba yake kwa jirani yake (Sa'ad) ili aishi kwa amani, upendo na mapatano.

Tofauti na Masahaba (Allah awaridhie), Waislamu wengi wa sasa tumekuwa wazito wa kufuata mafundisho ya Qur'an na Sunna za Mtume Muhammad (rehema za Allah na amani zimshukie). Badala ya viwili hivyo, tumekuwa tukifuata matamanio ya nafsi zetu. Na hii ndiyo tofauti iliyopo baina yetu na waja wema waliopita ambao walikuwa wakiwajali zaidi ndugu zao Waislamu kuliko nafsi zao.

## Usia wa Mtume

Tumeusiwa kuwatendea wema majirani, kuwapendelea kheri na kutowaudhi. Mtume wa Allah alikuwa mwema kwa majirani zake Waislamu na wasio Waislamu. Nao Masahaba (Allah awaridhie) wakarithi mwenendo huu kutoka kwa Mtume.

Imethibiti kwamba Abdullahi bin Umar (Allah amridhie yeye na baba yake) alichinja mbuzi kisha akawauliza watu wa familia yake: "Je, mmempa (nyama) huyu jirani yetu Myahudi? Hakika mimi nilimsikia Mtume (rehema za Allah na amani zimshukie) akisema, 'Jibril hakuacha kuniusia kuhusu jirani mpaka nikadhani kuwa atamrithisha (mali yangu).'" [Bukhari na Muslim].

## Wema unaofungamana na imani

Umuhimu wa kuwafanyia wema majirani unadhihiri katika kauli ya Mtume (rehema na amani ya Allah zimshukie) inayosema: "Anayemuamini Allah na Siku ya Mwisho, basi amkirimu jirani yake." [Bukhari na Muslim].

Hii inaonesha wazi kuwa kutowafanyia wema majirani ni jambo linalokwenda kinyume na mafundisho ya Uislamu. Tunajifunza katika hadith mbalimbali kwamba Mtume alikuwa akipenda kuwazuru majirani zake pindi wanapougua. Miongoni mwa majirani zake alikuwa Zaidu bin Arqam (Allah amridhie), ambaye amesema: "Nilipougua sikio Mtume (rehema za Allah na amani zimshukie) alikuja kunizuru." Mtume alikuwa akiwasaidia wagonjwa na kuwaliwaza pindi wanapofikwa na mitihani mbalimbali kadri alivyowezeshwa na Allah. Haya ndiyo yalikuwa maisha ya Kiongozi wa umma huu, Mtume Muhammad, ambaye Mwenyezi Mungu alimtuma ili awe mfano mwema wa kuigwa na walimwengu wote.

## Kujenga jamii imara

Tukio hili linatufundisha kujenga jamii bora inayojitambua na yenye kujali na kulinda maslahi ya watu wote. Na katika maslahi ya watu, utu ndiyo kitu chenye kutangulia. Mafanikio yetu hapa duniani na kesho Akhera yatatokana na kuwatendea wema majirani. Hii ni kwa sababu, mtu aliye karibu zaidi, ukiachilia mbali wazazi, jamaa na ndugu wa nasabu ni jirani.

Kuwatendea wema majirani ni pamoja na kuwapa chakula, kuwasaidia wakati wa matatizo na shida mbalimbali kama vile maradhi, msiba, kuvamiwa na wezi/ majambazi na kadhalika. Kutoka kwa Abu Dharr (Allah amridhie) amesema, Mtume (rehema za Allah na amani zimshukie) aliniambia: "Ewe Abu Dharr! Unapopika supu ongeza maji, kisha utazame jirani yako (kama anaihitajia)." [Bukhari na Muslim].

Katika riwaya nyingine, Abu Dharr amesema: "Hakika rafiki yangu, Mtume (rehema za Allah na amani zimshukie) ameniusia, 'Unapopika supu ongeza maji, kisha tazama kama baadhi ya majirani zako (wanahitajia), kisha wapelekee kwa wema.'" Hili ni jambo kubwa linalojenga upendo na mshikamano kwa majirani.

## Ubaya unapingana na imani

Kama tulivyotangulia kusema, kumtendea wema jirani ni moja kati ya mambo muhimu yanayokamilisha imani ya Muislamu. Kinyume chake ni kuwaudhi na kuwabughudhi majirani kunakopelekea imani kuporomoka.

Abu Huraira (Allah amridhie) amesimulia kuwa, mjumbe wa Allah (rehema na amani zimshukie) aliapa akasema: "Wallahi haamini! Wallahi haamini!" Masahaba wakauliza: "Nani ewe mjumbe wa Allah?" Akasema: "Yule ambaye jirani yake hasalimiki na shari zake." [Bukhari na Muslim].

IDARA YA DAAWA

**Mtume ﷺ amesema:**

"Muislamu ni yule ambaye Waislamu wengine wamesalimika kutokana na ulimi wake na mkono wake, na Muhajir (mhamaji wa kweli) ni yule anayeacha kile alichokataza Mwenyezi Mungu."

Bukhari

ربيع ثان

MAKALA
MALEZI

JUNAYNAT ALLY DAMA

# Qur'an, Hadith kama dira ya heshima kwa wazee

**"Na Mola wako amehukumu kwamba msimuabudu yeyote ila Yeye tu, na wazazi muwatendee wema. Wakifikia uzee mmoja wao au wote wawili ukiwa pamoja nao, basi usiwaambie hata 'ah!' wala usiwakemee, bali waambie maneno ya heshima." [Qur'an, 17:23]. Naye Mtume Muhammad (rehema za Allah na amani zimshukie) amesema: "Asiyewarehemu wadogo wetu, wala asiyetambua heshima na hadhi ya wazee wetu, si katika sisi." *[At-Tirmidhi; Abu Dawud].***



Hebu tuangalie maneno ya hekima ya watu kadhaa maarufu wakizungumzia umuhimu wa kuheshimu wazee katika jamii. APJ Abdul Kalam alisema:"Heshima kwa wazee ni sehemu ya mila zetu, na ni muhimu kuilinda (mila hiyo)."

Naye Nelson Mandela alikumbusha kuwa: "Wazee si raia wakongwe tu, ni walinzi wa mila, maadili na tamaduni zetu," huku Dalai Lama, kiongozi wa moja ya dini za kishirikina za huko Asia, Mabudha, naye akisisitiza, "Heshima kwa wazee ni ishara ya jamii iliyoistaarabika, na ni muhimu kuwafundisha watoto hilo."

Kwa upande wake, Rais wa zamani wa Marekani, Barack Obama alisema, "Hekima ya wazee ni hazina inayopaswa kuthaminiwa na kuheshimiwa." Malala Yousafzai anatoa wito, "Heshima kwa wazee ni sehemu ya ubinadamu wetu; tuwatendee kwa heshima, huruma na utu."

Umuhimu wa kuheshimu wazee

Kuheshimu wazee ni nguzo ya maadili ya jamii yenye ustaarabu, kwani wao ndio hazina ya kumbukumbu, tajiriba na busara zilizojaribiwa na muda. Heshima inayotolewa kwao hujenga dhamira ya pamoja, hurithisha stori za asili na maarifa ya familia, na kuunganisha vizazi kwa uaminifu na upendo.

Jamii inayowatunuku wazee heshima huwapunguzia upweke na kuwapa thamani ya utu wao wakati nguvu zao zimepungua. Wazee pia ni kielelezo kwa vijana juu ya namna ya kuishi maisha bora kwa kufuata nyendo zao na kujifunza walipokosea. Hatimaye, heshima hiyo huongeza thamani ya urithi wa kiutamaduni, huimarisha utambulisho wa pamoja, na hutengeneza mazingira salama ya kujifunza na kukua kwa vizazi vyote.

Mifano ya kivitendo ya heshima kwa wazee

Namna bora ya kuelezea kuhusu nini maana ya kuheshimu wazee ni kutaja mifano. Kwanza, kwenye kuheshimu wazee lazima kuwe na Ikhlas, yaani nia safi ya kutaka maslahi yao, si kujipendekeza.

Kuheshimu wazee ni kuenzi mamlaka zao na ikibidi kuhoji iwe kwa adabu na staha. Inahusisha kuwasikiliza kwa makini bila kuwakatiza, kuomba ruhusa kabla ya kutoa pingamizi, kutoa nasaha kwa upole pale panapohitajika na kuepuka kutoa lugha ya kejeli au kebehi dhidi yao.

Kuheshimu wazee pia kunajumuisha kuwapa kipaumbele katika jambo lolote kama kukaa kwenye viti, kula na kuwatanguliza kwenye foleni. Tunaweza kuandaa ratiba mahsusi ya kuwatembelea na kuwasikiliza, kisha kusajili historia zao za maisha kupitia sauti, maandishi au picha ili kizazi kijacho kijifunze.

Tunaweza pia kuwahusisha rasmi kama washauri wa familia katika maamuzi makubwa—kama mipango ya ndoa, miradi ya biashara au malezi—kwa kuweka vikao vya kusikiliza maoni yao kabla ya maamuzi kufanywa.

Ishara nyingine ya heshima ni kuwajengea upatikanaji rahisi wa huduma za msingi: kusaidia usafiri wa kliniki na ibada, kuweka miundombinu ya urahisi nyumbani kama mwanga wa kutosha, viti salama na njia zisizo na vikwazo, pamoja na kuwawekea vipindi vya mawasiliano ya kidijitali ili wabaki karibu na jamaa walio mbali. Pia tunaweza kuandaa siku maalumu za kusherehekea mafanikio yao kwa kutambua mchango wao shuleni, msikitini, kazini au kwenye mtaa.

Njia nyingine ya kuonesha heshima ni kulinda hadhi yao hadharani na faraghani, ikiwemo kutowatania kwa mambo yanayowaumiza. Tukiwapa nafasi za kufundisha ujuzi wao—kama bustani, ufundi, usimamizi wa fedha za kaya au mapishi ya jadi—tunawafanya wabaki kuwa wahusika hai, si watazamaji, huku tukijifunza stadi za maisha zinazodumu.

Mbinu ya kufundisha heshima kwa wakubwa

Katika familia na shuleni, tunaanza kwa kuwafundisha watoto maana ya mzee kwa kuwataja watu wanaostahili heshima hiyo. Tutaonesha mfano watoto kwa kuonesha namna ya kuwathamini wazee kwa vitu vidogo vidogo kila siku.

Nyumbani tunasisitiza kutopiga kelele mbele ya wazee, kuwajibu kwa heshima, kujenga utamaduni wa kuomba ushauri kwao. Kwenye jamii tunawahimiza vijana kuhudhuria mijadala kwa nidhamu, kutoa maoni kwa staha, na kujifunza namna ya kutofautiana na wazee bila kuvunjiana heshima.






UKHTI FATIMA SS

# Saikolojia ya giza: maana, mbinu 12 na madhara yake

**Saikolojia ya giza ni kutumia maarifa ya tabia na hisia za binadamu kudhibiti, kudanganya au kujeruhi wengine kwa maslahi binafsi. Si tawi rasmi la sayansi ya saikolojia, bali ni mbinu zisizo na maadili—kama udanganyifu, shinikizo la kihisia na uongo—zinazoweza kuonekana kwenye mahusiano ya kimapenzi, kazini, kwenye siasa, au hata mitandaoni.**
**Watu wenye sifa za ubinafsi uliopindukia, kutotahayari kuumiza wengine, tamaa au waliofunzwa mbinu za ushawishi bila uadilifu wanaweza kuzitumia. Kuelewa mbinu hizi hukuwezesha kutambua mapema alama hatarishi, kuweka mipaka, na kujilinda kiakili na kihisia.**

## Mbinu 12 za saikolojia ya giza

Moja ya mbinu za saikolojia ya giza kufanywa ujitilie shaka kumbukumbu au akili yako (gaslighting). Utaambiwa: "Hukusema hivyo," "Hukunielewa" ili tu kukuvurugia tathmini ya ukweli. Jikinge na hilo kwa kuandika matukio, kutafuta mashahidi na kuthibitisha hoja kwa vielelezo.

Mbinu ya pili ni kukutia hatiani ujisikie mkosefu (guilt-tripping) kama vile kusema "Kama ungenipenda kweli ungefanya kadhaa" hadi ukubali ombi la muhusika. Zuia hili kwa kuweka mipaka, kutoa majibu mafupi lakini thabiti.

Mbinu ya tatu kukumiminia mapenzi zawadi na sifa kwa kasi isiyo ya kawaida (Love bombing) ili kujenga utegemezi na baadaye hupunguzwa ghafla ili kukutawala. Zuia hili kwa kuangalia uthabiti wa tabia zao kwa muda, usiamini maneno pekee.

Mbinu ya nne ni kusifia kwa kukudhalilisha (negging), yaani kauli zenye kisu nyuma ya mgongo ili kukuondolea kujiamini. Atasema: "Unaonekana maridadi! Mimi sina ujasiri wa kutengeneza nywele hivyo," au "Bora ulivyoacha kuvuta sigara! Cha kusikitisha ni ushazeeka usoni." Fanya hivi: Kataa kutafuta kibali kwa mdhalilishaji, puuza maneno yake.

Mbinu ya tano ni ukweli nusu na kuficha kilicho muhimu ili kuunda taswira ya uongo (paltering). Jilinde kwa kutafiti na kuuliza maswali ya kuomba ufafanuzi yatakayomlazimisha muhusika afunguke ukweli wote. Taja kilichoachwa kwa makusudi, kama ushakijua.

Mbinu ya sita ni kumleta mtu wa tatu ili kuchochea wivu au shindano na hivyo kukutawala. Namna ya kujilinda na hili ni kuzungumza na mhusika pekee na epuka mijadala yenye "wasikilizaji" wasio wa lazima.

Mbinu ya saba ni kusambaza hofu (fearmongering) na kukuza tishio lisilo halisi ili ulazimike kutii. Mfano wa hilo ni kusema, "Fanya kitu una maadui wengi". Kukabiliana na hili, tafuta takwimu, uthibitisho huru, na jipe muda wa kutafakari kabla ya maamuzi.

Mbinu nyingine ni adhabu ya kimya (silent treatment). Lengo ni

kukunyima mawasiliano ili uombe radhi au utii. Ukiona hivyo, mueleze muhusika athari ya kimya na kamwe usikubali kufanya biashara ya hisia zako kwa hofu ya kutelekezwa.

Baadhi ya watu katika saikolojia ya giza hutumia mbinu ya 'kundi letu' (forced teaming) ili kukutwika majukumu yasiyo yako. Mathalan watasema "Sisi sote kazi tutafanya Jumapili, sivyo?" "Hakuna namna, itabidi tujitolee tu." Katika muktadha huo, unachotakiwa kufanya ni kubainisha majukumu. Pia, sema "Mimi naweza/siwezi" badala ya "sisi."

Mbinu ya kumi inaitwa "ushahidi wa kijamii" (social proof manipulation) ambayo inahusu kutengeneza

mapokeo au maoni ya bandia au ya uongo ili kukupindisha katika maamuzi. Kagua vyanzo, soma maelezo vizuri, linganisha chaguzi kupambana na mbinu hii.

Mbinu nyingine ya saikolojia ya giza ni chaguo bandia (restriction of choices) ikilenga kukusukuma uamue kati ya A au B ilhali zipo njia nyingi. Mtu atauliza, "Unanipenda au hunipendi" au "Unanipa sasa hivi au hunipi". Hapo hakuna chaguo jingine. Ukikabiliwa na hali hiyo, ongeza chaguo lako C. Uliza "Kwanini lazima iwe A au B tu?"

Mbinu ya 12 kukuza tatizo (amplifying problems) ambapo kosa dogo linaonekane janga kubwa ili mtu uchanganyikiwe na ukubali masharti ya mtwezaji. Askari wa barabarani mla rushwa anaweza kukuuliza: "Unajua kweli uzito wa kosa la kuvuka katika alama ya zebra?" Ukikabiliana na changamoto hiyo, pumua, chelewesha majibu, uzikubali ujazwe hofu, tathmini ukubwa halisi wa tatizo.

## Madhara ya saikolojia ya giza

Kiakili saikolojia ya giza huzalisha wasiwasi sugu, mfadhaiko, kujilaumu kupita kiasi, na kupungua kwa kujiamini, kiwewe, na usingizi mdogo. Kihisia na kijamii, hutengeneza upweke, utegemezi usio na afya, kuhisi kutengwa na marafiki/ndugu au aibu ya hadharani.

Mhanga pia, kitaalamu, hupata uchovu kazini na kufanya maamuzi mabovu chini ya shinikizo huku ubunifu na ufanisi nao ukishuka. Kimaadili na kiroho, ni wazi kunakosekana ukweli, uadilifu, huruma na uchamungu. Kifedha, ulaghai, mikataba mibovu, matumizi mabaya ya rasilimali ni matokeo ya saikolojia ya giza.

Mwisho, niseme kuwa saikolojia ya giza hustawi penye ujinga, haraka na ukimya. Jielimishe mbinu zake, ishi ndani ya mipaka yako, na usisite kuomba msaada.

NA UKHTI FATIMA



# Kumjali mteja ni zaidi ya huduma bora kwa mteja

Huduma kwa mteja (customer service) ni kile kinachoonekana wakati wa mawasiliano—kujibu maswali, kurekebisha makosa, kueleza taratibu. Kwa upande mwingine, kumjali mteja (customer care) ni falsafa pana zaidi: kuanza kumtazama mteja kama binadamu mwenye hisia na matarajio kabla, wakati na baada ya ununuzi.

Huduma mara nyingi hujibu tatizo lililopo; kumjali mteja hutabiri mahitaji, kujenga uhusiano wa kudumu na kuzuia matatizo yasitokee.

## Kwa nini kumjali mteja ni muhimu

Kila mawasiliano yanaweza kujenga au kuharibu sifa. Utafiti wa 2023 National Consumer Rage Study unaonyesha malalamiko kwenye mitandao ya kijamii yameongezeka maradufu tangu 2020. Hii ina maana tukio moja baya linaweza kuenea haraka na kudhoofisha chapa hata kama mara nyingi mnafanya vizuri.

Kuweka kumjali mteja kuwa kipaumbele hupunguza hatari, hujenga uaminifu, hupunguza kuhama kwa wateja na huongeza mapato. Wateja wako tayari kuacha maoni chanya pia kama utafiti wa BrightLocal 2025 unavyoonesha 64% ya wanunuzi wapo tayari kuandika tathmini nzuri wakipata uzoefu bora.

Na kumbuka hatari: takwimu za Zendesk Benchmark zinaonyesha 73% hubadilisha chapa baada ya matukio mabaya kadhaa, na zaidi ya 50% hubadilisha hata baada ya tukio moja baya. Kumjali mteja hufanya kosa lionekane la kibinadamu linaloweza kusameheka, si sababu ya kuondoka.

## Nguzo nne za kumjali mteja (4c's)

Huruma (Compassion) ni kuonyesha kwamba unaona na kusikia anachopitia mteja. Ruhusu ajieleze, thibitisha hisia zake, kisha toa suluhisho kwa staha. Mara nyingi, mteja anapotulizwa, hukubali hatua inayofuata kwa urahisi.

Uweledi (Competence) ni uwezo wa kutatua haraka na kueleza kwa uwazi tofauti ya kurejesha na kurekebisha, masharti ya dhamana, au chaguo mbadala. Uweledi hupunguza kurushiana mawasiliano na "kupigwa danadana".

Urahisi (Convenience) ni kufanya msaada upatikane kwa njia anazopendelea mteja—simu, WhatsApp, barua pepe, gumzo la papo hapo, duka au tovuti—na kwa wakati unaomfaa. Hakuna anayefurahia foleni ndefu au fomu zisizoisha.

Uthabiti (Consistency) ni kutoa kiwango kilekile cha kujali bila kujali kituo au mhudumu. Ukistahimili kiwango, mteja anatabiri kile atakachopata; hapo ndipo uaminifu huzaliwa.

## Nani anapaswa kushughulikia kumjali mteja

Wawakilishi wa huduma ndio mstari wa mbele, lakini kumjali mteja ni jukumu la wote. Muuzaji, masoko, fedha na utawala wote hukutana na mteja katika safari yake.

Sifa muhimu ni utu wa kusaidia, urafiki na huruma, kusikiliza kwa makini, maamuzi ya haraka na ubunifu wa kutatua matatizo.

Zaidi ya ujuzi, wahudumu wanapaswa kuakisi maadili ya kampuni—uaminifu, heshima na uwajibikaji.

## Jinsi ya kumjali mteja kazi

Anzisha utaratibu wa kusikiliza kwanza: rudia kilichosemwa kwa ufupi, kisha toa chaguo moja au mbili zilizo wazi. Eleza bei, muda, masharti na hatua zinazofuata kabla ya malipo ili kuepuka matarajio yasiyo halisi.

Fanya iwe rahisi kuwasiliana. Weka FAQ rahisi kusoma, chatbot yenye majibu sahihi, na namba au gumzo la kuonana na binadamu kwa masuala nyeti. Ukiwa haupo hewani, tumia ujumbe wa kupokea ombi (auto-acknowledgement) na muda wa makadirio ya majibu.

Wekeza kwenye ufuatiliaji. Baada ya suluhisho, tuma ujumbe mfupi: "Je, kila kitu kiko sawa sasa?" Hii huonyesha uwajibikaji, hupunguza kurudiwa kwa malalamiko, na hujenga kumbukumbu chanya.

Kusanya na tumia mrejesho. Fanya uchunguzi mfupi baada ya maingiliano, pitia maoni ya mitandao ya kijamii, na shiriki matokeo na timu. Onyesheni wazi mabadiliko mliyofanya kutokana na maoni ya wateja—hapo mteja huhisi sauti yake ina thamani.

Tumia teknolojia kwa busara. AI inaweza kusaidia kujibu maswali ya kawaida, kupendekeza hatua, au kubinafsisha mawasiliano kulingana na historia ya mteja. Lakini isichukue nafasi ya binadamu; iwaongezee wepesi na usahihi.

Tengeneza utamaduni wa ndani. Funza timu mara kwa mara kuhusu 4C's, tengeneza miongozo mifupi ya majibu, ruhusu maamuzi madogo ya mstari wa mbele (mfano, kuidhinisha kurejesha au punguzo dogo) ili kuepuka kuchelewesha suluhisho. Viongozi wasikilize simu/chaneli za wateja mara kwa mara ili kuona uhalisia na kuondoa vizuizi.

## Tofauti inayohisiwa

Kumjali mteja kunabadilisha huduma ya kawaida kuwa uhusiano wa muda mrefu. Unapoweka huruma, uweledi, urahisi na uthabiti kuwa mazoea, unalinda sifa yako, unapunguza adha ya malalamiko hadharani, na unaongeza uaminifu.

Mwisho wa siku, si tu tatizo lilivyotatuliwa, bali ni jinsi mteja alivyohisi alipotembelea chapa yako—hapo ndipo ushindani wa kweli unaamuliwa.